

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Ref.No.JA.9/259/01/A/38

22 Februari, 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Katibu wa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenyewe sifa na uwezo wa kujaza nafasi **moja (01)** kama ilivyoainishwa katika tangazo hili.

1.0 MWAJIRI: MKURUGENZI, HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO

1.0.1 MTEKNOLOJIA MIONZI (RADIOLOJIA) DARAJA LA II - (NAFASI 1)

1.0.2 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kuwapima wagonjwa wanaoelekezwa kwenye eneo la kazi .
- ii. Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia katika eneo lake la kazi.
- iii. Kukagua picha za X-Ray zilizopimwa kwa ubora na kutosheleza (Diagnostic Quality).
- iv. Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliowatumwa wagonjwa.
- v. Kusimamia watumishi walio chini yake.
- vi. Kutoa ushauri kuhusu masuala ya kazi za Radiolojia na Mionzi katika eneo la kazi.
- vii. Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa katika eneo

- lake la kazi (Sterilization).
- viii. Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi.
- ix. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

1.0.3 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia Mionzi (Radiolojia) ya muda wa miaka mitatu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale panapohusika.

1.0.4 MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani **TGHS.B**

MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. **Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.**
- iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayo jitoshaleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.
- v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
 - Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates.
 - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI
 - Computer Certificate
 - Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards)

- vi. **Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
- vii. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).**
- viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
- x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xi. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 07, Machi, 2022.**

Muhimu: Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vyta elimu. anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

KATIBU OFISI
YA RAIS
SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA
S.L.P. 2320 DODOMA.

- i. *Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo;*
<http://portal.ajira.go.tz/>

(Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa ‘**Recruitment Portal**’)

- ii. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**

Limetolewa na;

NAIBU KATIBU
SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA